**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**(SEKTA YA UVUVI)**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Uvuvi kupitia Mradi wa *South West Indian Ocean Fish (SWIOFish)*, inatangaza nafasi za Kazi za muda kwa ajili ya nafasi za Madereva kama ifuatavyo:

**Nafasi:** Dereva (Nafasi 3)

**Kituo cha Kazi:** Dar Es Salaam

**Kuripoti:** Mratibu wa Mradi SWIOFish

**Kazi:**

- Msimamizi wa majukumu yote aliyopewa katika kuhakikisha kuwa anafanya utekelezaji wa majukumu yake kwa wakati, ya kuendesha gari, usalama wa gari, utunzaji na matengenezo madogo na utoaji wa huduma bora za uchukuzi na usafirishaji kwa kazi za Mradi wa SWIOFish na kwa uaminifu na uadilifu;

- Kuendesha gari kwa mujibu wa kanuni za barabarani;
- Kufanya matengenezo madogo ya mitambo;
- Kuhakikisha gari inapelekwa kufanyiwa matengenezo kwa wakala wa huduma aliyeteuliwa na Mradi;
- Kutunza vitabu vya kumbukumbu za gari;
- Kufanya ukaguzi wa awali kwenye gari aliyopewa, kabla ya kusafiri na kutoa taarifa ya uharibifu au kasoro za mitambo;
- Kuhakikisha kuwa hati halali na vibali vinapatikana kabla ya kuanza kwa safari yoyote;
- Kutoa haraka taarifa za ajali au matukio yanayohusisha magari ya mradi kwa mamlaka husika; na
- Kuhakikisha usalama na usafi wa gari wakati wote.

**SIFA:**

- Cheti cha kufaulu elimu ya Sekondari

- Lazima awe na leseni halali ya kuendesha gari iliyotumika ndani ya miaka mitatu bila kusababisha ajali
- Uzoefu wa kuendesha magari katika sekta ya umma kwa muda usiopungua miaka 3.
- Cheti cha Trade Test Grade II/Driver Grade II Certificate kutoka NIT au VETA
- Sifa ya ziada itakuwa kwa Waliofaulu mafunzo ya Juu ya uendeshaji magari daraja la I (Advanced Drivers course grade I) na mafunzo ya Juu ya Udereva Hatua ya II ( Advanced Drivers course grade II)
- Ukomo wa Ummri: Miaka 18-50.

**MASHARTI YA AJIRA:** Mkataba wa Miezi 12

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI:** Kwa mwenye sifa zilizoanishwa hapo juu, tafadhali atume barua ya maombi ikiambatishwa na Wasifu wake ukionyesha majina ya wadhamini watatu (3), nakala za vyeti vya ufaulu wa elimu ya Sekondari,Vyeti vya Taaluma ya udereva pamoja na nakala mbili za picha ndogo (Passport size) za hivi karibuni. Waombaji watakaokidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye Usaili.

**Maombi yote yatumwe kwa barua pepe (barua@uvuvi.go.tz) kabla au ifikapo tarehe 31/07/2020** Kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu (UVUVI),
Wizara ya Mifugo na Uvuvi,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P. 2847,
**DODOMA.**